



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MDVC/ P.30/24/25/218

Tarehe : 20/03/2025

**NANINE BUSINESS ENTERPRISE**  
**MVOMERO**

**Yah: KUPEWA KIBALI CHA UJENZI WA JENGO LA KUHIFADHI MATUNDA NA MBOGAMBOGA (MULT STOREY BUILDING ) KATIKA ENEO LA DOMA KILOSA KATA YA DOMA.**

Rejea somo tajwa hapo juu.

2. Unajulishwa kuwa ombi lako limekubaliwa kupewa kibali cha Ujenzi wa Jengo la kuhifadhi matunda na mbogamboga (Mult storey Building) katika eneo la Doma Kilosa kata ya Doma.
3. Kwa barua hii, unatakiwa kufanya ujenzi kwa Mujibu wa Kanuni na Taratibu za kibali kilichotolewa ikiwa ni pamoja na kuheshimu mipaka ya barabara, hifadhi mbalimbali na kuhakikisha unatunza miti ya asili.
4. Kimsingi kibali hicho kitadumu kwa muda wa miezi sita (6) kuanzia tarehe ya barua hii na kama hakitatumika hakitaruhusiwa kutumika tena, unapaswa kuomba kibali kingie. Aidha, unatakiwa kutoa taarifa ya utekelezaji kwa kila hatua iliyofikiwa, na Ofisi ya Mhandisi wa Ujenzi (W) itafanya ukaguzi wa kila hatua kama fomu ya ukaguzi inavyoelekeza.

Nakutakia kazi njema.

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO  
S.L.P. 663

Loema P. Isaay,

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**  
**MVOMERO.**